**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. PHILIP ISDOR MPANGO, MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KATIKA MBIO ZA CRDB MARATHON 2022, DAR ES SALAAM

**VIWANJA VYA FARASI**

**14 AGOSTI 2022**

***Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, pamoja na Mheshimiwa Mama Salma Kikwete (Mb);***

***Mheshimiwa Mussa Azan Zungu (Mb.), Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;***

***Waheshimiwa Mawaziri mliopo mkiongozwa na Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa (Mb), Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo;***

***Mheshimiwa Amos Makala, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam;***

***Dkt. Ally Hussein Laay, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Benki ya CRDB;***

***Ndugu Abdulmajid Nsekela, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB;***

***Waheshimiwa Mabalozi na Wakuu wa Mashirika ya Kimataifa mliopo;***

***Viongozi wote wa Chama na Serikali;***

***Menejimenti na Wafanyakazi wote wa Benki ya CRDB;***

***Profesa Mohamed Janabi, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete;***

***Bi. Brenda Msangi, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya CCBRT;***

***Viongozi wa Taasisi mbalimbali;***

***Wageni wetu wote kutoka nchi za Nje;***

***Wadau wote waliofanikisha mbio hizi ambao ni pamoja na Taasisi ya Sanlam, Clouds Media na Taasisi ya Bima ya Strategis;***

***Washiriki wote wa Mbio hizi za hisani;***

***Ndugu Wanahabari, Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana***

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania……CRDB Marathon 2022 oyee!!**

Awali ya yote, namshukuru mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema kuweza kushiriki kwenye Mbio hizi za hisani za mwaka huu 2022 zijulikanazo kama CRDB Marathon 2022. Kwa niaba ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na watanzania wote, napenda kuwakaribisha wageni wote kutoka nje ya nchi waliokuja kushiriki nasi. *We warmly welcome to Tanzania all our guests from other countries who have come to join us in this gracious event.*

Nimefurahi sana kuona mwitikio mkubwa wa wananchi na wadau wengi kushiriki mbio hizi za hisani. Hii inadhihirisha kukubalika kwa mbio hizi na pia utayari wa wananchi pamoja na wadau mbalimbali kuwa sehemu ya suluhisho katika utatuzi wa changamoto zilizopo kwenye jamii yetu. Hivyo, sisi kama viongozi wa Serikali hatuna budi kuwashukuru na kuwaunga mkono. Asanteni sana.

***Waheshimiwa Viongozi wote mliopo***
***Wananchi na Wageni Waalikwa;***

Kipekee kabisa, naomba nikushukuru sana Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Bwana Abdulmajid Nsekela kwa kunialika kuja kushiriki katika Mbio hizi. Aidha, naupongeza Uongozi mzima wa Benki ya CRDB, wanahisa, Bodi ya Wakurugenzi, Wadhamini, Wafanyakazi wa Benki hii pamoja na wadau wote waliohusika kuandaa na kufanikisha mbio hizi muhimu sana. Nawashukuru kwa dhati Benki ya CRDB kwa ubunifu huu wa kuandaa mbio hizi za hisani, *CRDB Bank Marathon*, ambazo zinafanyika kwa mwaka wa tatu mfululizo kwa mafanikio, huku mkizidi kushirikisha wadau mbalimbali kuchangia fedha za kusaidia maeneo yenye uhitaji mkubwa katika jamii yetu. Nimependa sana kuona watanzania wengi pamoja na wageni marafiki zetu, mmejitokeza kuchangia watoto wetu ili waweze kupata huduma za upasuaji wa moyo kupitia ushiriki wenu kwenye *CRDB Bank Marathon*. Hivi sasa, Taasisi yetu ya Moyo ya Jakaya Kikwete inaweza kuhudumia watoto 250 hadi 300 kwa mwaka ambayo ni sawa na asilimia 10 tu ya mahitaji yote ya nchi kwa mwaka. Gharama za upasuaji na kuhudumia mtoto mmoja ni kati ya Shilingi milioni mbili (2,000,000) hadi Shilingi milioni kumi na moja (11,000,000) ikitegemea ukubwa wa tatizo. Mtakubaliana na mimi kuwa gharama hizi ni za juu sana kwa Mtanzania wa kawaida. Kwa takwimu zilizopo, hadi kufikia mwezi Juni mwaka huu 2022, Hospitali imekuwa na wagonjwa takribani 750 ambao wanahitaji kufanyiwa upasuaji mkubwa na mdogo wa moyo. Hii inadhihirisha ni kwa kiasi gani fedha hizi mnazochangia zinahitajika sana.

Nimefurahishwa pia na uamuzi wa *CRDB Bank* kutumia *Marathon* ya mwaka huu kuchangisha fedha kwa ajili ya akina mama wenye ujauzito hatarishi ili wapate huduma stahiki katika Hospitali ya CCBRT ambayo ni mdau mkubwa wa Serikali kwenye kuboresha utoaji huduma za mama na mtoto. Ijapokuwa kwa sasa hakuna takwimu maalum kuonesha idadi ya wanawake wenye ujauzito hatarishi, sisi sote ni mashahidi kuwa miaka ya hivi karibuni kumekuwa na uhitaji mkubwa wa huduma za dharura kwa mama mjamzito katika kipindi cha ujauzito au kujifungua. Tumeshuhudia kinamama wengi pamoja na watoto wakipoteza

maisha kutokana na mimba hatarishi. Changamoto kubwa kwenye upatikanaji wa huduma hii ni upungufu wa watalaam wenye sifa stahiki katika ngazi zote za huduma nchini hususan kwenye huduma za afya ngazi ya msingi. Hivyo michango yenu itaokoa maisha ya kinamama wengi pamoja na watoto wao. **Asanteni sana.**

***Waheshimiwa Viongozi wote mliopo***
***Wananchi na Wageni Waalikwa;***

Mbio hizi za hisani zinatupatia nafasi nyingine sisi upande wa Serikali kushirikiana na wadau, taasisi na sekta binafsi katika kutafuta suluhu ya changamoto mbalimbali kuhusu upatikanaji wa huduma za jamii hapa nchini. Benki ya CRDB imekuwa mstari wa mbele katika utoaji wa huduma za fedha na misaada ya kijamii. Mbali na kutengeneza fursa za ajira, biashara na ujasiriamali, kupitia mbio hizi za hisani, Benki ya CRDB imeweza kutoa takriban Shilingi bilioni 1 kusaidia wananchi wa kipato cha chini kupata matibabu katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete. Aidha, fedha hizo pia zimewezesha uanzishwaji wa kituo cha kisasa cha taarifa na huduma kwa wagonjwa katika Taasisi ya Saratani ya Ocean Road. Kadhalika, fedha hizo pia zimetumika katika uhifadhi na utunzaji wa mazingira yetu kupitia kampeni ya "Pendezesha Tanzania". Tunawapongeza sana sana Benki ya CRDB pamoja na wachangiaji wote kwa jitihada hizi njema.

***Waheshimiwa Viongozi, Wananchi na Wageni Waalikwa;***

Mazoezi ya mwili ni muhimu sana kwa afya njema. Aidha, maendeleo ya nchi yetu yanahitaji nguvukazi yenye afya njema. Hata hivyo, Watanzania wengi, hususan wanaoishi mijini, wanakabiliwa na hali ya uzito uliozidi (overweight). Inasikitisha kuona kuwa vijana wengi siku hizi wanapoteza maisha kutokana na magonjwa yasiyo ya kuambukiza kama vile kisukari na shinikizo la damu; magonjwa ambayo kwa kiasi kikubwa husababishwa na mtindo wa maisha, ulaji usiofaa na kutofanya mazoezi mara kwa mara. Nafurahi kupitia mbio hizi, Benki ya CRDB mnaelimisha watanzania juu ya kutunza afya, uwepo wa magonjwa yasiyoambukizwa, jinsi ya kuyatambua, kujikinga pale inapowezekana na upatikanaji wa tiba. Nawasihi sana hata baada ya leo, muendelee kuhimiza watanzania wote kuishi maisha yanayofuata misingi ya afya bora, kuendelea kufanya mazoezi pamoja na kuwa na bima ya afya. Aidha, napenda kuwasihi watanzania wenzangu, utaratibu wa kufanya mazoezi uwe ni wa kudumu kwa kila mmoja ili kujiepusha na maradhi na pia kujipunguzia sisi wenyewe pamoja

na Serikali mzigo mkubwa wa gharama za matibabu ya magonjwa yanayoweza kuepukika kwa kufanya mazoezi mara kwa mara.

***Ndugu Viongozi, Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana***

Uamuzi wa Benki ya CRDB kusajili mbio hizi Kimataifa ni mzuri kwa sababu unatoa fursa kwa wanariadha wetu kufikia muda wa kukimbia unaotambulika Kimataifa na hivyo kuwawezesha kushiriki mbio za kimataifa. Ni uamuzi ambao pamoja na faida nyingine, umesaidia pia kuziba hilo ombwe lililokuwepo katika tasnia yetu ya michezo. *Tunawashukuru na kuwapongeza sana.* Kupitia mbio hizi sasa tutaungana na "Kili marathon" kupokea watalii wa kimichezo kutoka nchi mbalimbali ambao pamoja na kukimbia, watapata pia fursa ya kuona vivutio vya utalii vilivyopo nchini pamoja na fursa za biashara na uwekezaji. Napenda niwahakikishie kuwa Serikali itaendelea kuwaunga mkono na kushirikiana nanyi ili kuhakikisha hiki mlichokianzisha kinaleta tija zaidi katika tasnia ya michezo na hata kiuchumi pia.

***Waheshimiwa Viongozi wote mliopo***
***Wananchi na Wageni Waalikwa;***

Pamoja na mafanikio mengi tuliyoyapata kupitia Mbio hizi za CRDB Marathon, bado kuna changamoto nyingi zinazoikumba jamii yetu. Naomba nitumie fursa hii, kutoa rai kwenu Benki ya CRDB pamoja na taasisi nyingine za kifedha, wadau wa maendeleo, taasisi za umma na sekta binafsi kuisaidia Serikali kupambana na changamoto zifuatazo:

**Jambo la kwanza,** ambalo ningependa kusisitiza hapa ni kuhusu lishe. Kufanya mazoezi ni jambo jema lakini haitoshi. Ni lazima pia kula chakula bora na cha kutosha chenye virutubisho ambavyo ni msingi wa afya njema. Lakini kiuhalisia hali ya Afya na Lishe miongoni mwa Watanzania hususan baadhi ya akina mama wajawazito na watoto chini ya umri wa miaka mitano bado sio ya kuridhisha. Hii ina maana kuwa, tusipochukua hatua, baada ya miaka kadhaa tutakuwa na Taifa lenye nguvukazi ya watu wenye uwezo mdogo wa kufikiri na tija ndogo katika kazi za aina zote! Hivyo naomba nitumie fursa hii kutoa wito kwenu Benki ya CRDB, mabenki mengine na taasisi mbalimbali nchini kusaidiana na Serikali kutoa elimu ya lishe kwa jamii yetu pamoja na kuhamasisha kufanya mazoezi kama hivi leo.

**Jambo la pili,** ambalo ningependa mtupie jicho, ni kuhusu kusaidia watoto wanaozaliwa kabla ya wakati (Watoto Njiti). Ijapokuwa tatizo hili hutokea bila ya

sababu maalum (*spontaneous delivery*), lakini wakati mwingine husababishwa na ujauzito wa mapacha, magonjwa ambukizi na magonjwa ya muda mrefu kama kisukari na shinikizo la juu la damu. Hapa nchini, takwimu zinaonesha kuwa, kwa mwaka, watoto laki mbili (200,000) huzaliwa kabla ya wakati na kati ya hao takribani watoto elfu tisa mia tano (9,500) hufariki ndani ya kipindi cha mwaka mmoja baada ya kuzaliwa. Hii ni sawa na asilimia 4.75 ya watoto wote wanaozaliwa kabla ya wakati. Serikali inaendelea kuboresha na kuimarisha huduma za watoto njiti, lakini katika vituo vyetu vya kutolea huduma za afya bado kuna upungufu wa vifaa tiba vya kusaidia watoto hawa. Hivyo, naomba kutoa wito kwenu pamoja na taasisi nyingine, kushirikiana na Serikali kukabiliana na changamoto hii. Aidha, nawaomba pia muwekeze katika kutoa elimu ya afya ya uzazi hasa vijijini ili kukabiliana na ongezeko la watoto njiti katika jamii yetu.

***Waheshimiwa Viongozi wote mliopo***
***Wananchi na Wageni Waalikwa;***

**Jambo la Tatu,** ni suala la mabadiliko ya tabianchi duniani na uhifadhi wa mazingira. Suala la mazingira ni mojawapo ya vipaumbele muhimu vya Serikali ya Awamu ya Sita. Serikali inatambua na kupongeza mchango wa Sekta binafsi, pamoja na wadau katika kuunga mkono juhudi za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kutunza na kuhifadhi mazingira hapa nchini. Hata hivyo, pamoja na juhudi zote, bado tatizo ni kubwa. Mbali na ongezeko la gesijoto kutokana na shughuli za viwandani, mabadiliko ya tabianchi na uchafuzi wa mazingira huchangiwa kwa kiasi kikubwa na shughuli za binadamu, yaani tabiawatu, kama kukata miti hovyo; kuchoma misitu; kutupa takataka hovyo kwenye vyanzo vya maji na nchi kavu; kilimo cha kuhamahama; ujenzi holela; na ufugaji usiozingatia tija. Hapa nchini tumeshuhudia madhara ya mabadiliko ya tabianchi ikiwa ni pamoja na ukame wa muda mrefu, mvua zisizotabirika, na hata kusababisha kutoweka kwa mazingira asilia. Athari hizi pia zinaleta changamoto kwenye uzalishaji katika sekta zetu za kilimo, uvuvi pamoja na ufugaji. Ili kukabiliana na changamoto hii, hatuna budi kutunza mazingira yetu kwa kupendezesha miji yetu na kufanya usafi; kulinda vyanzo vya maji; kulinda misitu na kupanda miti kwa wingi ili kupunguza ongezeko la Hewa Ukaa, na hivyo kuongeza upatikanaji wa hewa safi.

Nafahamu Benki ya CRDB imekuwa ikishirikiana kwa karibu na Ofisi yangu ambayo ina jukumu la kusimamia utunzaji na uhifadhi wa mazingira hapa nchini. **Tunawashukuru na kuwapongeza sana!** Hivyo, naomba nitumie fursa hii kuzisihi taasisi nyingine za kifedha na wadau wengine kuunga mkono juhudi hizi

hasa katika kuhamasisha, kukuza uelewa na kujenga uwezo wa jamii na taasisi mbalimbali katika kuhifadhi mazingira yetu. Serikali inaendelea na kampeni kote nchini kujanisha na kupendezesha miji yetu. Sasa natoa wito kwenu, mtuunge mkono. Kwa kufanya hivyo mtachangia juhudi za Serikali katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na pia kutekeleza mikataba ya kimataifa kama Mkataba wa Kyoto (*Kyoto Protocol*) 2005; na Mkataba wa Paris (*Paris Agreement, 2015*). Nina imani kwamba tukiunganisha nguvu zetu, hili linawezekana.

**Jambo la nne na la mwisho**, kama mtakumbuka, wakati wa uzinduzi wa Jengo la Makao Makuu ya Benki ya CRDB, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alisisitiza na kuzitaka taasisi za kifedha nchini kuiwezesha sekta binafsi ishiriki katika kilimo, hasa cha umwagiliaji ambacho ndiyo kipaumbele cha Serikali kwa mwaka huu wa fedha. Nawapongeza Benki ya CRDB kwa kuitikia wito na kuwa wa kwanza kutoa kwa wakulima mikopo ya riba nafuu ya asilimia 9 pamoja na kushirikiana na Wizara ya Kilimo kuweka miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya kimkakati yaliyoandaliwa katika mikoa mbalimbali. Nafahamu pia mnawawezesha wajasiriamali, wamachinga pamoja na wale walio katika makundi maalum kupata elimu ya biashara zao, mikopo nafuu pamoja na kuwatafutia masoko. Hili ni jambo jema na la kupongezwa. Napenda nitoe rai kwa taasisi nyingine za fedha kuiga mfano huu na kumuunga mkono Mheshimiwa Rais. Aidha, ninazitaka tena benki zetu kuangalia tena uwezekano wa kupunguza zaidi riba ya mikopo ili kuwawezesha wananchi kukopa na kurejesha mikopo yao kwa wakati. Naamini bado inawezekana kupunguza.

***Ndugu Viongozi, Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana***

Napenda nihitimishe hotuba yangu kwa kuwapongeza kwa mara nyingine tena Benki ya CRDB kwa mafanikio yaliyopatikana kutokana na Mbio hizi na pia utendaji wa Benki kwa ujumla. Mafanikio haya yote yanaashiria uwepo wa mazingira mazuri ya kiutendaji na mahusiano thabiti ya kibiashara.

**Mwisho**, naomba kuwakumbusha pia wananchi wote kuwa tarehe 23 Agosti 2022 ni siku ya Sensa ya Watu na Makazi. Nawaomba wananchi wote tujitokeze kuhesabiwa na kutoa kila aina ya ushirikiano utakaohitajika kufanikisha zoezi hili muhimu kwa mipango ya maendeleo ya Taifa letu.

**Mungu Ibariki Tanzania.**

**Asanteni sana kwa kunisikiliza.**